BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 13 Septemba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 27 Juni, 2023.

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

48. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Wabunifu kutoka katika kundi la Watu Wenye Mahitaji Maalum wanaweza kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa letu.

    (a) Je, ni kazi ngapi za ubunifu za Watu Wenye Mahitaji Maalum zimepokelewa.

    (b) Je, Wizara ipo tayari kiasi gani kupokea kazi mbali mbali za wabunifu hao ambao miradi yao imekwama kwa kukosa ufadhili.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

84. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Serikali kwa makusudi kabisa ilitunga Sheria ya Kudhibiti Vileo, Namba 9 ya mwaka 2020 kwa lengo la kudhibiti uingiaji na matumizi ya vileo Zanzibar. Hata hivyo, athari chanya za sheria hiyo hazijaonekana katika jamii.

(a) Je, ni ipi tathmini ya Serikali kwenye madhumuni na kufuatwa vilivyo sheria hii.

(b) Je, kuna changamoto gani katika utekelezaji wa sheria hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

8. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa mpango maalum wa kudhibiti mapato ya nchi kwa njia ya kudai risiti za kielektroniki kwa chochote kile ambacho utanunua. Hata hivyo kuna baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta (Sheli) bado haziko tayari kufuata mpango huo maalum wa Serikali.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kudhibiti upotevu wa mapato kwa sheli ambazo mwananchi anapodai risiti za kielektroniki baada ya kutia mafuta, hujibiwa kuwa hamna risiti hizo.

(b) Je, wananchi wasiopewa risiti hizo wachukue hatua zipi wanapokumbana na hali hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

68. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kazi kubwa ya kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu. Katika jitihada hizo, wanafunzi waliomo katika jimbo la Uzini nao wanafaidika na elimu inayotolewa na Wizara hii. Hata hivyo, wanafunzi hao wanakabiliwa na tatizo la kukosa vyeti vyao vya kumalizia masomo (Leaving Certificates).

Je, kwa nini wanafunzi wa jimbo la Uzini hawajapata “Leaving Certificate” zao za kumalizia masomo kuanzia mwaka 2020 hadi 2023.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

42. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wabunifu ndio chachu ya maendeleo kwa taifa lolote lile duniani.

(a) Je, Wizara yako inawafahamu wabunifu wepi waliopo Zanzibar ambao kazi zao zimekuwa na mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya uchumi, sayansi na teknolojia nchini mwetu.

(b) Je, Wizara yako inawaenzi na kuwasaidia vipi wabunifu hao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

9. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa inapendekezwa kwenye maeneo yote yanayotoa huduma za kijamii kuwa na huduma za vyoo vya wanawake na wanaume, na kwa kuwa Boti ya Kilimanjari VII ina vyoo vinne (4) vyote vya jinsia moja.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu jambo hilo.

(b) Je, Wizara yako inachukua hatua zipi kuhakikisha kuwa vyoo vilivyomo katika boti ya Kilimanjaro VII, vinatofautishwa kijinsia.

**Wizara ya Afya:**

75. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Kiembesamaki kipo katika hali mbaya sana na hatarishi kwa wauguzi na wagonjwa wanaokwenda kupata huduma ya afya kituoni hapo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondosha changamoto katika Kituo hicho cha afya cha Kiembesamaki.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

28. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Je, Taasisi ya Kilimo na Utafiti (ZARI) kupitia kitengo chake cha Sayansi ya Chakula na Lishe kina mikakati yoyote ya kuwaelimisha wananchi juu ya uelewa wa elimu ya lishe.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais,Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**13 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**